THE GUARDIAN Page 11



Kisesa legislator Luhaga Mpina, who is also Livestock and Fisheries minister, greets Meatu residents when he toured the district yesterday for a first-hand account of the ongoing construction of a secondary school in Isengwa ward. Photo: Guardian Correspondent

Scanned by CamScanner

na virusi vya corona. Hatua hii ni utekelezaji wa tatu mfululizo yaliyotangazwa wachache watahudhuria maombi vya haban,"

MAJIRA UK 3



Mbunge wa Jimbo la Kisesa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, akihakiki taarifa zake kwenye Daftari la Kudumu la Wapikura katika Kata ya Lubiga, Wilaya ya Meatu, Mkoa wa Simiyu. Kulia ni ofisa mwandikishaji Joseph Mkongola. (Na Mpigapicha Wetu)

## Wach madi kuny

Na Patr Kaham

Scanned by CamScanner



**MAZUNGUMZO: Mbunge wa Viti Maalumu, Rhoda Kunchela (Chadema) akizungumza na Mbunge wa Kilolo, Venance Mwamoto (CCM) nje ya Ukumbi wa Bunge Dodoma juzi.**

MTANZANIA UK 17.

# *Mbunge ataka suluhu migogoro ya wafugaji*

MBUNGE wa Viti Maalumu, Rhoda Kunchela (Chadema) amehoji migogoro ya muda mrefu kati ya hifadhi na wafugaji Serikali inachukua hatua gani kuitatua.

Pia amehoji Serikali inachukua hatua gani kwa baadhi ya askari wanyamapori wanaofanya uonevu unaokiuka sheria mbalimbali kwa wafugaji nchini.

Akiuliza swali jana bungeni, Kunchela alisema kumekuwepo na migogoro ya muda mrefu kati ya hifadhi na wafugaji nchini hali inayosababisha jamii ya wafugaji kupata madhara mbalimbali ikiwemo vifo, uonevu, mifugo kutaifishwa na kutozwa faini zinazokiuka sheria za nchi.

"Je, Serikali inawatambua wafugaji waliopata madhara hayo, Serikali inachukua hatua gani kwa baadhi ya askari wanyamapori wanaofanya uonevu huu unaokiuka sheria mbalimbali kwa wafugaji nchini," aliuliza Kunchela.

Ikijibu, Wizara ya Maliasili na Utalii ilieleza kuwa kwa nyakati tofauti wafugaji ambao wamekuwa wakiingiza mifugo yao ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa wamekuwa wakikamatwa na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Ilieleza utaratibu unaotumika kuwakamata wafugaji hao mara zote unazingatia sheria na taratibu zinazosimamia maeneo ya hifadhi.

Wizara hiyo ilieleza kuwa askari wa wanyamapori wamekuwa wakifanya kazi zao kwa kufuata sheria za nchi katika ulinzi wa rasilimali za taifa.

Aidha, Serikali imekuwa ikitoa msisitizo kwa watumishi hao kufuata sheria na taratibu kuwakamata wale wote wanaoingiza mifugo ndani ya maeneo yaliyohifadhiwa ikiwa ni pamoja na kuwafikisha katika vyombo vya sheria. Wizara ilieleza kuwa katika ukamataji wa wahalifu hao taratibu za kisheria zinafuatwa.

Hata hivyo, kwa nyakati tofauti kumekuwa na matukio ya wafugaji kuvamia vituo vya askari na kuwashambulia kwa silaha za jadi kwa lengo la kuchukua mifugo yao, suala ambalo ni kinyume na sheria za nchi. "Kwa mfano, katika Hifadhi ya Taifa Ruaha mnamo tarehe 09/10/2018, askari wanyamapori mmoja aliuawa na wananchi waliovamia kituo kiitwacho Nyota kwa lengo la kukomboa mifugo yao iliyokuwa imekamatwa baada ya kuingizwa kinyume na utaratibu," wizara ilieleza.

Aidha, katika hifadhi hiyo hiyo, Julai 3 mwaka 2016, askari mwingine wa wanyamapori aliuawa na wananchi waliovamia kituo cha Ikoga kwa lengo la kukomboa mifugo yao. "Askari wa wanyamapori wanaobainika kukiuka sheria, kanuni na taratibu, wizara imekuwa ikiwachukulia hatua stahiki za kinidhamu kulingana na sheria, kanuni na taratibu za kiutumishi.

"Katika kuendelea kutafuta suluhisho la uingizaji wa mifugo ndani ya hifadhi, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika maeneo yanayozunguka hifadhi kadiri bajeti itakavyoruhusu.

za utoaji les
huduma za
mwaka 201
za fedha za
2015 zinaip
Tanzania k
ya malipo
Ilielez
zinazotoa
zinapewa
kanuni hi
riba vina
midogo
kampun
ya soko
nyingin
mikopo
ambapo
unatum
riba ki

Ma

Scanned by CamScanner